TANGAZO LA SERIKALI Na 435 la tarehe 31/10/2014

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287 R.E. 2002)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)

SHERIA NDOGO ZA (KILIMO KWANZA NA HIFADHI YA CHAKULA) ZA HALMASHAURI YA NGARA ,2014.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kilimo Kwanza na Hifadhi ya Chakula) za ,Halmashauri ya Wilaya ya Ngara,2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Ngara

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapohitajika vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Mtendaji wa Kata au Kijiji, pamoja na mtumishi yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Afisa Ugani" maana yake ni mtaalamu wa kilimo, mifugo Uvuvi na Nyuki katika ngazi za vijiji, mitaa na kata.

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

"Kilimo" maana yake ni shughuli yoyote ya uzalishaji mali inayofanywa na binadamu na itajumuisha kilimo cha mazao, ufugaji wa wanyama hai, nyuki na samaki.

"Maji ya asili" maana yake ni bahari, maziwa, mabwawa ya asili, mito pamoja na mabwawa yasiyo ya asili ambayo uvuvi wa umma unafanyika;

"Mazao" maana yake ni Mazao yote yanayolimwa ndani ya Halmashauri.

"Mifugo" maana yake ni utunzaji wa wanyama hai ufanywao na binadamu na utajumuisha nyuki na samaki.

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Halmashauri na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri na haitamhusu mtu yeyote;

(a) mwenye umri chini ya miaka 18;
(b) asiyejiweza kutokana na ulemavu, kuugua au uzee;
(c) Mwanafunzi aliyeko masomoni muda wote.

"Mkulima" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na uzalishaji au kilimo cha mazao ya chakula, biashara na matunda.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Skimu za Umwagiliaji" maana yake ni miundombinu ya miradi ya maji ambayo imeanzishwa na Serikali au Halmashauri na kuwapa wananchi ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

"Uhawilishaji" maana yake ni kitendo cha uzalishaji wa wanyama kwa njia ya kisasa kwa kutumia mbegu za madume bora ili kupata kizazi kipya cha wanyama bora.

"Uvuvi haramu" maana yake ni uvuvi unaotumia zana zisizokubalika katika uvuvi kama mabomu, sumu, makokoro, mikuki na vyandarua.

"Uvuvi holela" maana yake ni uvuvi usio na leseni wala kibali cha Halmashauri.

"Vyanzo vya Maji" maana yake ni mito, vijito, maji yanayotiririka, visima, mabwawa, mifereji, maziwa, chemi chemi au ardhi oevu.

"Wagani kazi" maana yake ni wananchi ambao wamepata mafunzo ya ugani nje ya vyuo ili kufanya kazi za maafisa ugani pale ambapo hawapo.

"Zana haramu" maana yake ni vyandarua, mabomu, sumu, makokoro, nyavu zisizokubalika kitaalam pamoja na mikuki.

SEHEMU YA PILI
KILIMO CHA MAZAO

Wajibu wa Halmashauri

4 Katika kuhamasisha na kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza Halmashauri itakuwa na wajibu wa;-

(a) kuhakikisha viongozi wa Serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wanashiriki

ipasavyo katika kuendeleza sekta ya kilimo katika Halmashauri;

(b) kuunda vikundi vya sanaa vinavyohamasisha kilimo cha kisasa;

(c) kuweka mabango kwenye kila kijiji yanayoeleza kanuni bora za kilimo yanayopaswa kuzingatiwa na mkulima kwa mazao yanayolimwa kwenye eneo hilo

(d) kuanzisha mashamba darasa ya mfano katika kila kijiji

(e) kuhakikisha upatikanaji rahisi na kwa wakati wa pembejeo za kilimo

(f) kutekeleza mipango ya msimu wa kilimo unaofuata mara baada ya mwisho wa msimu;

(g) kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani katika kila kijiji;

(h) Kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya wakulima vya kuweka na kukopa kwa lengo la kujipatia mikopo ya benki.

(i) kuanzisha vituo vya kukuzia na kufundishia wanyama kazi

(j) kuanzisha vituo maalum kwa ajili ya kutolea mafunzo ya utumiaji na utunzaji wa zana bora za kilimo;

(k) kuhamasisha matumizi ya wanyama kazi katika maeneo ambayo wafugaji hujishughulisha pia na kilimo cha mazao;

(l) kushindanisha wakulima bora na maafisa ugani bora katika vijiji,kata na hatimaye Halmashauri;

(m) kuanzisha mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani

(n) kuainisha matumizi bora ya ardhi ghalani ili kubainisha na kutofautisha ardhi ya mifugo,kilimo na hifadhi ;

(o) kusimamia upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine za kilimo;

(p) kusimamia upatikanaji, maadili na mwenendo wa mawakala wa mbolea na pembejeo za kilimo;

(q) kuhamasisha Serikali za vijiji na wananchi kwa ujumla kujenga maghala ya chakula ya vijiji;

Wajibu wa serikali ya kijiji

5 (1) Serikali ya kijiji inatenga ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo, maeneo ya ufugaji wa nyuki mabwawa ya kufugia samaki.

(2) Serikali ya kijiji kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji itahakikisha kuwa kila mkazi anapata ardhi ya kutosha kwa ajili yakutekeleza kauli mbiu ya kilimo kwanza;

(3) Serikali ya kijiji kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kila mkazi wa kijiji anajitosheleza kwa chakula;

(4) Kila mkazi katika eneo la kijiji anayemiliki ardhi ya kilimo chini ya sheria yeyote ile na mwenye uwezo wa kufanya kazi, atatakiwa kulima mazao ya chakula na biashara.

Wajibu wa Afisa muidhiniwa

6 Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mkulima;-

(a) anaandaa mashamba kwa wakati;
(b) anapanda mbegu kwa mstari;
(c) anazingatia nafasi inayotakiwa kitaalam;

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(d) anaweka mbolea kwa viwango na kwa wakati;
(e) anapalilia kwa wakati palizi mbili au zaidi;

Hifadhi ya mazao

7 (1) Kila mkazi atakayelima shamba katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuvuna mazao yake pindi yakisha komaa na kuyahifadhi katika njia ya usafi ili kutunza ubora wake na kuhifadhi katika njia ya usalama

(2) Itakuwa ni jukumu la kila mkazi hususani mkuu wa kaya kuhakikisha kuwa anahifadhi chakula cha kutosha yeye na familia yake kwa angalau mwaka mmoja au zaidi.

(3) Litakuwa ni jukumu la kila kaya kuwa na ghala la kuhifadhia chakula ambalo litapaswa kuwa katika hali ya usalama na lisiwe na uwezekano wowote wa kuruhusu wadudu kama vile dumuzi, panya au wadudu wengine wanaoweza kuingia na kusababisha uharibifu wa chakula hicho

Wajibu wa kulima

8 Kila mkazi anayemiliki au atakayemilikishwa shamba kwa mujibu wa kifungu cha 5 (1) cha Sheria Ndogo hizi atawajibika kulilima, kulitunza na kuendeleza shamba lake kwa mujibu wa maelezo ya kitaalamu atakayopewa na Afisa Ugani.

9 Bila kuathiri kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo hizi itakuwa ni wajibu wa kila Mkulima:-

(a) kupalilia shamba kabla ya wakati wa mavuno isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo;
(b) kuweka mbolea;
(c) kutoa taarifa kwa Halmashauri kwa njia itakayokuwa inafaa kuhusu kuwepo kwa ugonjwa wa mazao au kuwepo kwa wadudu waharibifu;

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(d) kutumia pembejeo kwa kuzingatia maelezo ya kitaalamu kila mwaka isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Afisa Ugani;

(e) kuchukua hatua za kuangamiza wadudu waharibifu au kutibu magonjwa kama atakavyokuwa ameelekezwa na Afisa Ugani.

(2) Kila Afisa Ugani atawajibika kutoa programu ya kilimo ya mwaka kulingana na hali ya hewa;

(a) programu hiyo itazingatia aina ya mazao kwa msimu;

(b) aina ya mbegu kwa msimu husika;

(c) namna na wakati wa kupanda

Ukaguzi 10 Afisa mwidhiniwa akishirikiana na Afisa Ugani;-

(a) ataweza wakati wowote wa saa za kazi kuingia kwenye eneo la kilimo au katika shamba kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

(b) ataweza kuingia katika kaya yoyote ili kukagua ghala la chakula kuona kama taratibu za kuhifadhi chakula zinazingatiwa;

(c) ataweza kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi;

(d) atatakiwa kuwa na daftari linaloonyesha idadi kamili ya wakazi na idadi ya ekari zao za kilimo;

(e) atapanga ratiba ya kutembelea mashamba ya wakazi ili kujionea kama wanatekeleza wajibu wa kulima na kutunza mashamba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

11 Kila Afisa Mtendaji wa kata au Kijiji atawajibika kutunza kumbukumbu za mashamba yote ya mazao yaliyomo katika Kata au Kijiji chake na atasimamia moja kwa moja utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

12 Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote;

(a) anayemiliki ardhi ya kilimo kushindwa au kukataa au kukataza shamba hilo kulima mazao ya chakula,biashara au matunda;
(b) kutotunza shamba;
(c) kutovuna mazao yaliyoko shambani ambayo yamefikia wakati wa kuvunwa;
(d) kutokuwa na ghala la kuhifadhia mazao au kutolitumia;
(e) kutohifadhi chakula cha kutosha;
(f) kuuza mazao bila kuweka akiba ya mwaka mzima au zaidi;
(g) kuuza mazao yakiwa shambani;

SEHEMU YA TATU
UFUGAJI WA KISASA

Wajibu wa Halmashauri

13 Ili kuendeleza ufugaji bora na wa kisasa Halmashauri itakuwa na majukumu yafuatayo;-

(a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kutenga maeneo ya wakulima, wafugaji na maeneo ya hifadhi;
(b) kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani;
(c) kuhakikisha upatikanaji wa madawa ya mifugo na chanjo za mifugo;
(d) kuhakikisha uwepo wa majosho katika kila kijiji au kitongoji kwa kushirikisha nguvu za wananchi;
(e) Kuanzisha kamati za majosho kwenye kila kijiji au kitongoji ambapo majosho hayo yameanzishwa.

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(f) kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mifugo hai na nyama;

(g) kuanzisha minada na magulio ya mifugo ndani ya maeneo ya Halmashauri na kuhimiza wafugaji kutumia minada hii ili kuvuna na kupunguza idadi ya mifugo;

(h) kuhamasisha wananchi kuanzisha vyama vya ushirika wa wafugaji na vyama vya kuweka na kukopa;

(i) kusaidia kuanzisha vituo vya uhawilishaji wa mifugo ili kupata madume bora ya kisasa na mifugo yenye tija;

(j) kushindanisha wafugaji vijijini, mitaa na kata ili kupata washindi wa mfugaji bora wa mwaka katika mtaa,kijiji na katika kata kwa mwaka;

(k) kushindanisha maafisa ugani wote katika vijiji na kata ili kumpata afisa ugani bora katika ngazi za vijiji,mitaa,kata na Halmashauri;

(l) kuandaa vigezo vya kuwapata maafisa ugani bora wa mifugo katika vijiji,mtaa na kata;

(m) kutoa zawadi za kijiji, mtaa, na kata bora katika ufugaji kwa mwaka;

(n) kutoa zawadi kwa mfugaji bora kwa mwaka wa kila kijiji,mtaa,kata na Halmashauri;

(o) kutoa zawadi kwa afisa ugani bora wa mwaka kila Halmashauri, kata, mtaa au kijiji;

(p) kutoa zawadi kwa shamba darasa la mifugo kwa mwaka;

(q) kuhakikisha upatikanaji wa mabwawa ya maji ya kunyweshea mifugo;

(r) kuhakikisha upatikanaji rahisi wa soko la ngozi za mifugo;

(s) kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogovidogo vya mazao ya mifugo kama mikanda,pochi,mapambo yatokanayo na ngozi za wanyama na usindikaji wa

maziwa,siagi,jabini na mtindi;

(t) kuanzisha klabu za wanywaji maziwa katika Halmashauri;

(u) kufanya uperembaji wa mara kwa mara juu ya ufugaji wa kisasa ili kujadili mafanikio na udhaifu katika utekelezaji ili kuweza kuboresha au kuimarisha au kurekebisha kosoro zilizojitokeza;

(v) kuhamasisha wafugaji wa vijijini kuanzisha mashamba ya mazao ya kilimo ili wanufaike na upatikanaji rahisi wa mbolea ya mboji;

(w) kuhamasisha wafugaji kufanya uvunaji wa mara kwa mara wa mifugo ili kubakisha idadi ndogo ya mifugo yenye kuleta tija na rahisi kuihudumia;

(x) kuanzisha machinjio ya wanyama ambayo ni ya kisasa na salama ili kurahisisha uvunaji wa mifugo kwa njia ya uchinjaji;

(y) kuhakikisha udhibiti wa ufugaji wa kuhamahama ili kuhifadhi mazingira.

(z) kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii ili kudumisha amani,utulivu na maelewano katika jamii za wakulima na wafugaji;

Wajibu wa serikali ya kijiji

14 Serikali ya kijiji kwa ushirikiano na uongozi wa kitongoji itahakikisha;

(a) inaandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(b) kila mfugaji anapata ardhi ya kutosha ya malisho ya mifugo;

(c) inasimamia na kulinda mipaka ya ardhi ya kilimo na mifugo iliyobainishwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi;

(d) inatoa au kutaja idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji ataruhusiwa kuwa nayo;

(e) inasimamia uanzishwaji wa majosho ya mifugo kwa ushirikiano na wafugaji;

(f) inahamasisha wafugaji kuvuna mifugo

yao mara kwa mara ili kubakisha idadi ya mifugo yenye kuleta tija;

(g) wataalamu wa ugani waliopo katika kijiji wanatoa elimu ya ufugaji wa kisasa ili kupata mifugo bora na mazao bora ya mifugo;

Wajibu wa Afisa Mwidhiniwa

15 Afisa Mwidhiniwa au Afisa Ugani atatakiwa;-

(a) kuwa na daftari linaloonyesha idadi kamili ya mifugo kwa kila mfugaji;
(b) kuingia katika kaya yoyote ili kukagua aina na idadi ya mifugo;
(c) kuhakikisha kuwa mfugaji anachanja na kuogesha mifugo yake mara kwa mara ili kuepuka magonjwa ya mifugo;
(d) kuhakikisha kuwa mfugaji mwenye mifugo iliyozidi anavuna mifugo hiyo;
(e) kutoa taarifa kwa Halmashauri mara anapogundua kuna mlipuko wa magonjwa ambayo yanahitaji msaada kutoka ngazi za juu;
(f) Kumchukulia hatua mfugaji yeyote anayekwenda kinyume na masharti ya ufugaji yaliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

Wajibu wa Mfugaji

16 (1) Kila Mfugaji atahakikisha anafuga idadi ya wanyama ambayo haitasababisha usumbufu kwa wadau wengine wa kilimo kama ilivyoidhinishwa kwenye kibali cha Halmashauri;

(2) Atalazimika kuchanja mifugo yake kila mara ili kuzuia magonjwa ya mifugo na magonjwa ya mlipuko.

(3) Atalazimika kuogesha mifugo yake ili kuihami dhidi ya magonjwa,kupe na mbung'o.

(4) atalazimika kujiunga na vyama vya wafugaji wajasiriamali.

(5) atalazimika kutoa taarifa yoyote juu ya kutokea kwa magonjwa ya mifugo akiyaona au kuhisi au kuyatambua dhidi ya mifugo yake.

(6) (a) atalazimika kulishia au kuchungia mifugo yake katika maeneo yaliyotengwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Halmashauri.

(b) atalazimika kufugia mifugo yake ndani ya banda (zero grazing) kwa idadi ambayo Halmashauri itatoa kibali.

(7) atalazimika kuheshimu mipaka iliyotenganisha ardhi ya kilimo,mifugo,hifadhi za Taifa ,makazi,maeneo ya Taasisi na maeneo mengine ya wadau wa kilimo kama mazao ya wakulima, wafugaji wa nyuki, samaki na skimu za umwagiliaji;

(8) atashirikiana na maafisa mifugo au maafisa ugani wakati wa tiba au chanjo wakati wa magonjwa ya mlipuko na karantini na kampeni zozote za kitaifa za kudhibiti magonjwa na vifo vya mifugo.

(9) atashirikiana na maafisa ugani kuanzisha mashamba darasa na mashamba ya kulishia mifugo

(10) ataheshimu masharti ya karantini wakati wa magonjwa ya mlipuko;

Uvunaji wa mifugo

17 (1) Kila mfugaji atawajibika kuvuna mifugo yake kila atakapobaini kuwa imevuka idadi iliyoko kwenye kibali kilichotolewa na Halmashauri.

(2) Wakati wa uvunaji wa mifugo kila mfugaji ataweza kuuza wanyama hai au kwa kuchinja na kuuza nyama.

(3) Kabla ya kuvuna mfugaji atashirikiana na afisa mifugo ili kujiridhisha kwamba wanyama wake hawana maradhi wala magonjwa ya kuambukiza.

Makosa

18 Mfugaji yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;-

(a) atashindwa kuvuna mifugo iliyozidi idadi iliyoko kwenye kibali kilichotolewa na Halmashauri au;

(b) atashindwa au kukataa kuchanja mifugo yake ili kuzuia magonjwa au;

(c) atalisha mifugo yake kwenye maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo au;

(d) ataruhusu mifugo yake kuzurura hovyo; au

(e) atazembea au kushindwa kutoa taarifa juu ya ugonjwa wa mifugo au;

(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Afisa Ugani kutekeleza majukumu yake au;

(g) atasafirisha mifugo pasipokuwa na kibali cha Halmashauri na;

(h) atasafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

SEHEMU YA NNE
SKIMU ZA UMWAGILIAJI

Jukumu la Halmashauri

19 (1) Halmashauri itaanzisha skimu za umwagiliaji katika maeneo ya vijiji ambayo upatikanaji wa maji siyo wa shida ili kuchochea kilimo cha umwagiliaji;

(2) Skimu za umwagiliaji zilizoanzishwa na Halmashauri zitagawiwa kwa wanavijiji ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji;

(3) Halmashauri zitaendelea kutoa utaalam wa ugani na matumizi bora ya skimu hizi ili kuzifanya ziwe endelevu;

(4) Miundombinu iliyopo kwenye skimu za umwagiliaji itaendelea kuwa chini ya umiliki wa Halmashauri;

(5) Halmashauri itawajibika kufanya ukarabati wa miundombinu katika skimu isipokuwa kwa uharibifu wa makusudi au uzembe utakaosababishwa na matumizi mabaya ya skimu;

(6) Halmashauri itagawa skimu kwa wananchi watakaoomba na kuahidi kutunza skimu hizo ili ziwe endelevu;

(7) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumfutia kibali mtu yeyote ambaye atathibitika kutumia vibaya skimu au ataharibu au atakodisha kwa mtu mwingine bila ridhaa ya Halmashauri;

(8) Halmashauri itashindanisha watumiaji wa skimu za umwagiliaji ili kumpata mshindi atakayejulikana kama "mtunzaji na mtumiaji bora wa skimu" mshindi huyo atapewa zawadi na Halmashauri;

(9) Halmashauri itatoa leseni ya utumiaji wa skimu na itakuwa na uwezo wa kubatilisha leseni hiyo.

(10) Kabla ya kupewa leseni mwombaji atalazimika kulipa ada ya utunzaji skimu (Scheme Maintanance Fee) itakayopangwa na Halmashauri, ada hiyo italipwa kila mwaka na mwombaji ataruhusiwa kulipa kwa awamu mbili kwa mwaka;

(11) Maafisa wa Halmashauri watakuwa na uwezo wa kuingia kwenye skimu saa yoyote wakati wa saa za kazi ili kufanya ukaguzi;

(12) Pasipo kuathiri kifungu cha 19(11) maafisa wa Halmashauri watakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi baada ya saa za kazi na siku za mapumziko au jumamosi na jumapili au siku za sikukuu ili mradi wawe na kibali cha Mkurugenzi;

Wajibu wa watumiaji skimu za umwagiliaji

20 Watumiaji wa skimu za umwagiliaji watakuwa na majukumu yafuatayo;-

(a) kutunza, kulinda, kuhifadhi na kuheshimu miundombinu iliyoko katika skimu za umwagiliaji;

(b) kutoa taarifa za uharibifu wa miundombinu ya skimu kila inapotokea;

(c) kulipia leseni na ada za skimu kila mwaka;

(d) kujiunga na umoja wa skimu au chama cha watumiaji wa skimu katika skimu ambayo wao ni watumiaji;

(e) kufanya ukarabati wa skimu kwa uharibifu ambao umesababishwa na uzembe au matumizi mabaya ya miundombinu ya skimu;

(f) kulipa fidia ya gharama kwa Halmashauri endapo Halmashauri itafanyia ukarabati uharibifu uliosababishwa na watumiaji au wanachama wa skimu;

(g) kuwaruhusu maafisa wa Halmashauri na kuwapa ushirikiano wakati wowote wanapotaka kuingia au kukagua miundombinu ya skimu;

(h) kushirikiana na Halmashauri wakati wowote kunapotokea haja ya kuboresha miundombinu ya skimu ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwenye skimu;-

(i) katika kufanya hivyo watumiaji watatakiwa kuchangia nguvu kazi au fedha taslimu;na

(ii) Umoja wa watumiaji wa skimu utachangia rasilimali fedha kutoka katika akiba yake

(i) watumiaji wa skimu za umwagiliaji watabuni vyanzo vya mapato na kuweka taratibu za namna ya kukusanya ili kuwa na hazina ambayo itatumika kama italazimika kufanya hivyo ili kuboresha

au kuimarisha miundombinu ya skimu za umwagiliaji;

(j) kulinda vyanzo vya maji ambavyo vinaingiza maji katika skimu za umwagiliaji;-

(i) Katika kufanya hivyo mtu yeyote; hataruhusiwa kuchepusha maji kwa sababu yoyote au kwa namna yoyote bila ruhusa ya Halmashauri;

(ii) Hataruhusiwa kupanda miti au mimea yoyote ambayo inaweza kusababisha hasara au uharibifu au kuhatarisha miundombinu ya skimu au kupunguza kina cha maji katika skimu.

Barabara za Halmashauri

21 Bila kuathiri majukumu ya Halmashauri yaliyoainishwa katika vifungu vya 4, 13 na 19, Halmashauri itahakikisha kwamba barabara za Halmashauri zinapitika ili kurahisisha usafirishaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo na mazao wakati wa mavuno.

Marufuku ya jumla

22 (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi;

(a) kusafisha au kuandaa shamba kwa kuchoma moto;

(b) kuchoma moto msitu wa hifadhi;

(c) kulima katika vyanzo vya maji,miteremko au misitu ya hifadhi;

(d) kuchunga na kunywesha mifugo katika vyanzo vya maji au miteremko au misitu ya hifadhi;

(e) kulima kando kando ya barabara au hifadhi za barabara za vijiji,Wilaya,Mikoa au Taifa;

(f) Kuswaga mifugo barabarani au kuchungia mifugo barabarani au kandokando ya barabara au katika hifadhi ya barabara.

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(2) Bila kuathiri masharti yaliyopo kwenye kifungu cha 22(1) (a) mtu yeyote anaweza kuruhusiwa kusafisha au kuandaa shamba kwa kuchoma moto baada ya kuomba na kupata kibali maalumu kutoka kwa Halmashauri;

(3) Halmashauri itatoa kibali baada ya Afisa Mwidhiniwa kuridhika kwamba taratibu zote za kuzuia moto usilete madhara zimezingatiwa ikiwa ni pamoja na;

(a) kutengeneza wigo mpana kati ya shamba litakalochomwa moto na mashamba jirani ili moto usivuke au kuenea kwenye mashamba hayo au misitu;
(b) kutoa taarifa ya angalau siku saba kabla ya kuchoma moto kwa majirani wanaozunguka shamba hilo;
(c) kuwepo kwa taarifa ya angalau siku saba kwa serikali y a kijiji kabla ya kuchoma moto;

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina, tarehe, eneo analotaka kuchoma moto na maoni ya Halmashauri.

Makosa

23 (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;-

(a) ataharibu miundombinu iliyopo kwenye skimu za umwagiliaji; au
(b) atashindwa kukarabati miundombinu ya skimu kwa uzembe au matumizi yake mabaya ya miundombinu hiyo; au
(c) atashindwa au atakataa kulipia leseni na ada ya skimu; au
(d) atachepusha maji kutoka kwenye vyanzo vya maji bila kibali cha Halmashauri au;

(e) atapanda miti au mimea inayoweza kusababisha hasara, kuhatarisha au kuharibu miundombinu ya skimu

(2) Bila kuathiri maelezo ya kifungu cha 33 endapo kosa alilotenda mtu huyo lilisababisha hasara au uharibifu wa mali ya kijiji au Halmashauri au Serikali au skimu ya umwagiliaji au mali ya mtu binafsi; ataamriwa kufanya matengenezo au kulipa fidia ya matengenezo na akishindwa atahukumiwa kifungo cha miezi kumi na miwili jela.

SEHEMU YA TANO
UFUGAJI WA SAMAKI NA UVUVI

A. UFUGAJI WA SAMAKI

Ufugaji

24 Halmashauri kulingana na jiografia yake,sayansi ya udongo wake,upatikanaji wa maji na mvua itakua na wajibu wa kuhamasisha, kuanzisha na kusimamia ufugaji wa samaki wa kisasa katika eneo lake

Jukumu la Halmashauri

25 Ili kutekeleza mahitaji ya kifungu cha 29 cha Sheria Ndogo hizi itakuwa ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha kwamba;

(a) inahamasisha wananchi juu ya uanzishaji wa kilimo cha ufugaji wa samaki;
(b) inaanzisha mabwawa ya mfano ya samaki katika kila kata;
(c) inawezesha upatikanaji wa maafisa ugani wa uvuvi kwenye kata na vijij;
(d) Vifaranga vya samaki vinapatikana ili kupandikizwa katika mabwawa ya wananchi, Kata, Vijiji, na Vitongoji.

Jukumu la serikali ya kijiji

26 Ili kutekeleza azma na dhamiri ya kuhamasisha ufugaji wa samaki kila Serikali ya kijiji itahakikisha kwamba;

(a) inatenga ardhi ya kuanzishia mabwawa ya mfano au mashamba darasa ya ufugaji wa samaki;
(b) inaanzisha mabwawa ya samaki ya kijiji ili kukuza kipato cha makusanyo ya

maduhuli ya kijiji;

(c) inaanzisha vyama vya kuweka na kukopa vya wafugaji wa samaki kijijini;

(d) inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya kuanzisha mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusiana na ufugaji bora wa samaki;

(e) Inaanzisha masoko na minada maalum katika siku maalum kwa ajili ya kuuzia samaki.

Jukumu la Afisa uvuvi

27 Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila Afisa uvuvi wa kata au kijiji atakuwa na jukumu la;

(a) kuanzisha rejesta ya orodha ya wafugaji wote wa samaki katika kata au kijiji;

(b) kupanga ratiba ya kuwatembelea wafugaji wa samaki katika kata au kijiji;

(c) kuanzisha orodha na idadi ya mabwawa ya samaki na aina ya samaki katika kila bwawa katika kata au kijiji;

(d) kuanzisha mashamba darasa au mabwawa ya mfano kwa ajili ya kutolea mafunzo ya nadharia na vitendo;

(e) kuhakikisha upatikanaji wa vifaranga na mbegu bora ya samaki;

(f) kuanzisha programu ya kuangamiza samaki wakubwa wanaowala samaki wadogo (predators) katika mabwawa;

(g) kuanzisha programu ya kuangamiza magugu maji katika mabwawa;

(h) kuandaa programu ya uendelezaji na ukuzaji wa kilimo cha ufugaji wa samaki katika kata au kijiji;

(i) Kuhakikisha wafugaji wa samaki wanatumia nyavu sahihi wakati wa kuvuna katika mabwawa yao ili kutoharibu mazalia na kutovuna samaki wadogo.

B. UVUVI KATIKA MAJI YA ASILI

Uvuvi katika maji ya asili

28 Wananchi watakuwa na ruhusa ya kuvua katika maji ya asili kama mito, maziwa, mabwawa ya asili na yasiyo ya asili na bahari kwa vibali maalum vya uvuvi.

Jukumu la Halmashauri

29 Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba;-

(a) wavuvi wote wanakuwa na vibali na leseni halali za uvuvi;
(b) wavuvi wanatumia nyavu zinazokubaliwa kitaalam
(c) inapiga marufuku uvuvi haramu wa kutumia makokoro,sumu, mabomu na vyandarua;
(d) inatoa elimu ya uvuvi wa kisasa na zana za uvuvi zinazokubalika kisheria;
(e) inaanzisha vikosi vya wananchi vya kupambana na wavuvi haramu kupitia ulinzi shirikishi;
(f) inaanzisha masoko na minada ya samaki katika fukwe za maji ya asili na yasiyo ya asili;
(g) inateketeza zana haramu za uvuvi zinazotengenezwa na wavuvi haramu;
(h) inawafikisha wavuvi haramu katika vyombo vya dola kwa hatua za kisheria pindi wanapokamatwa;
(i) vijiji vyote vinavyopakana au kuzungukwa na maji ya asili vinapatiwa maafisa uvuvi;
(j) inaanzisha vikosi vya doria katika fukwe zote za maji ya asili ili kupambana na uvuvi haramu;
(k) inaandaa mpango wa kuwazawadia raia wema wanaotoa taarifa kuhusu wavuvi haramu;

(l) inatenga na kuanzisha makambi ya wavuvi ili kuzuia uvuvi holela na uvuvi haramu;

(m) inafanya ukaguzi wa leseni za uvuvi wa mara kwa mara na kuwachukulia hatua wavuvi wasio na leseni;

(n) itaanzisha na kutunza rejesta ya orodha ya wavuvi wote wenye leseni katika Halmashauri;

(o) itahakikisha kwamba wavuvi wote halali wanalipa ushuru wa kisheria kwa Halmashauri;

(p) inahamasisha wavuvi kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa ili kuweza kujipatia mikopo katika mabenki kwa ajili ya kukuza mitaji na kujipatia zana bora na za kisasa za uvuvi;

30 (1) Chini ya Sheria Ndogo hizi Halmashauri itakuwa na uwezo wa kusitisha, kufuta au kumnyang'anya leseni endapo itabaini uvunjifu wa masharti ya leseni ya uvuvi.

(2) bila kuhatarisha maelezo ya kifungu cha 30 (1) hapo juu pamoja na kuwa na uwezo wa kusitisha au kufuta au kunyanganya leseni Halmashauri itaweza kuangamiza au kuteketeza kwa namna yoyote ile inayo ona inafaa zana haramu zilizokamatwa na kutelekezwa na wamiliki wake,

(3) Halmashauri itakamfikisha mahakamani mtu yoyote atakaye kamatwa akiendehsa uvuvi haramu.

Jukumu la Afisa uvuvi

31 Kila Afisa uvuvi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa Kata, Kijiji na Mtaa atakuwa na wajibu wa;

(a) kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

(b) kuhamasisha na kuunda vikosi vya doria dhidi ya wavuvi haramu;

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(c) kufanya ukaguzi wa leseni mara kwa mara katika makambi ya wavuvi;

(d) kutoa elimu juu ya uvuvi salama, uvuvi endelevu na hifadhi ya mazingira katika maeneo ya uvuvi;

(e) kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaokiuka Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote andishi ya uvuvi na hifadhi ya mazingira;

(f) kuanzisha na kutunza rejesta yenye orodha ya wavuvi katika kata, kijiji na mtaa;

(g) kuanzisha rejesta yenye majina ya makambi ya uvuvi, idadi ya makambi na idadi ya wavuvi katika makambi hayo;

SEHEMU YA SITA

KUTHIBITI UGONJWA WA MNYAUKO WA MIGOMBA(UNYANJANO)

Jukumu la Mkulima

32 (1) Kila mkulima wa zao la migamba anawajibika kuhakikisha kuwa wakati wote hakuna mgomba wenye ugonjwa wa unyanjano katika shamba lake

(2) Mkulima atawajibika kung'oa mgomba wowote utakaoonekana kuwa na dalili za ugonjwa wa unyanjano na kufuata maelekezo yote yanayotolewa au yaliyotolewa na maafisa ugani.

(3) Kila mkulima au mmiliki wa shamba la migomba atahakikisha kuwa anatoa taarifa kwa afisa ugani au kiongozi wake wa Serikali juu ya uwepo wa ugonjwa wa unyanjano katika shamba lake.

(4) Litakuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki, akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi Hamsini

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

elfu(50,000/=) na isiyozidi shilingi laki tatu(300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Makosa

33 Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo;

(a) atavua samaki kwa kutumia mabomu au milipuko au sumu au mikuki;
(b) atavua bila kuwa na leseni halali;
(c) atakataa au kukwepa kulipa ushuru wa Halmashauri;
(d) atatumia nyavu zisizokubaliwa kitaalam;
(e) atauza samaki katika maeneo yanayokatazwa chini Sheria Ndogo hii au sheria yoyote andishi;
(f) ataendesha shughuli za uvuvi bila kujiandikisha kweshe rejista ya wavuvi ya kata, kijiji au mtaa;
(g) atavua katika maeneo ya hifadhi au eneo lolote lisiloruhusiwa kisheria;
(h) atapatikana akivua au akiuza samaki wodogo wadogo.

Adhabu

34 (1) Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi sita jela au adhabu zote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) endapo mtu huyo atapatikana na hatia kwa kosa la kuvua au kumiliki zana haramu za uvuvi au nyavu zenye matundu yasiyokubalika kisheria, pamoja na adhabu ya kifungo au faini au kifungo na faini mahakama itaamuru vitu hivyo viteketezwe.

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

Sheria Ndogo hizi (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara zimetungwa kwa Azimio la Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 5 mwezi Mei 2013 na Mhuri wa Halmashauri umebandikwa mbele ya:-

JOHN M. SHIM'IMANA
Mwenyekiti Halmashauri Wilaya ya Ngara

CORNEL E. NGUDU-NGI
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ngara

NAKUBALI

Dodoma
27 Juni, 2014

MIZENGO P. PINDA (MB),
Waziri Mkuu

)

TANGAZO LA SERIKALI Na. 436 la tarehe 31/10/2014

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA ZA MWAKA ,2014

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za(Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara za mwaka, 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali

Matumizi

Tafsiri

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo maneno yafuatayo yatakua na maana ya;-

“Halmashauri “ maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ngara;

“Mazao” maana yake ni mazao yatokanayo na Kilimo na Maliasili.

“Ushuru wa Mazao” maana yake ni kiwango cha fedha kinachopangwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kutoza

“Mazao” maana yake ni mazao yatokanayo na Kilimo na Maliasili.

Maeneo

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

ya kuuzia mazao

4. Mazao yote yanayotokana na kilimo yatauzwa na wakulima katika maeneo maalum yaliyopangwa na Serikali za Vijiji kwa madhumuni hayo yakiwemo maeneo ya Vyama vya Msingi.

Kosa

5. Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kununua mazao nje ya maeneo yaliyopangwa na Serikali na Vijiji pamoja na maeneo yaliyowekwa na Vyama vya Msingi isipokuwa kwa mazao yafuatayo:-

a) Ndizi ;
b) Vitunguu;
c) Muhogo;
d) Mbogamboga; na
e) Mazao ya Maliasili

Wajibu wa kulipa Ushuru

6. (1)Kila mnunuzi anayenunua mazao kwa misingi ya kufanya biashara anawajibika kulipa ushuru wa mazao kwa Halmashauri kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali.

(2)Kila mtu anayenunua mazao kwa madhumuni ya biashara anapaswa kuwa na Leseni.

Ulipaji wa Ushuru

7. (1). Ushuru uliotajwa katika jedwali la Sheria Ndogo utalipwa na mtu anayetakiwa kulipa ushuru huo katika kituo au kijiji cha manunuzi ya zao husika, isipokuwa mazao ya Kahawa na ufuta Ushuru utalipwa Makao Makuu ya Wilaya.

(2). Ushuru wa mbao na magogo utalipwa katika kijiji ambapo mazao hayo yamenunuliwa.

(3). Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru katika kituo au kijiji cha manunuzi, atalazimika kulipa ushuru huo pamoja na adhabu ya Asilimia hamsini (50%) ya ushuru huo.

Adhabu

8. Mtu yeyote atayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilling elfu hamsini(50,000) au kifungo cha miezi sita jela, au adhabu zote mbili kwa pamoja yani faini na kifungo.

JEDWALI

Na.	Zao	Ushuru
1	Kahawa	Asilimia tano (5%) ya bei kwa kilo moja
2	Alizeti	Asilimia tano (5%) ya bei kwa kila moja
3	Mahindi	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
4	Parachichi	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
5	Karanga	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
6	Vitunguu	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
7	Kunde	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
8	Mtama	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
9	Njugu	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja la kilo 100
10	Mpunga/Mchele	Shilingi 1,000/= kwa kila gunia moja
11	Muhogo	Shilingi 500/= kwa kila gunia moja
12	Ndizi	Shilingi 300/= kwa kila mkungu moja
13	Nyanya	Shilingi 500/= kwa kila tenga moja
14	Mbao	Shilingi 500/= kwa kila ubao
15	Mazao mengine	Shilingi 500/= kwa kila gunia moja

Sheria Ndogo hizi zimetungwa kwa Azimio la mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 5 mwezi Mei 2013 na Mhuri wa Halmashauri Umebandikwa mbele ya:-

JOHN M. SHIM'IMANA
Mwenyekiti Halmashauri Wilaya ya Ngara

CORNEL E. NGUDU-NGI
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya
Wilaya ya Ngara

NAKUBALI

Dodoma
27 Juni, 2014

MIZENGO P. PINDA (MB),
Waziri Mkuu

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)
TANGAZO LA SERIKALI Na. 437 la Tarehe 31/10/2014

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))

_____

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA ZA MWAKA, 2014

SEHEMU YA I
UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara za Mwaka, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo;-

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"**Halmashauri**" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Madini ya ujenzi" maana yake ni Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Maegesho'' Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.

"Mazao ya misitu'' maana yake ni mazao yote yatokanayo na misitu iliyoko katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na mazao hayo ni pamoja na mbao,kuni,mkaa, fito,nguzo,asali,nta,ukindu,katani,magamba ya miti,majani,mizizi,vinu,mitwangio,mipini mikuki na fagio.

"Masoko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa.

"Mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa.

"Mnada wa mifugo'' maana yake ni mnada wa Lumasi Kata ya Kasulo,Murusagamba,Rulenge pamoja na eneo lingine litakaloteuliwa na Halmashauri kuwa mnada..

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

"Ushuru wa Madini ya Ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa Kokoto, Mawe, Changarawe, Mchanga, Chokaa, Marumalu, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika Mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

SEHEMU YA II
NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-

i. Ada ya kukodisha mali za Halmashauri,
ii. Ada ya machinjio, ukaguzi wa nyama na ushuru wa Bucha,
iii. Ushuru wa Mazao mchanganyiko,
iv. Ushuru wa stendi na maegesho,

v. Ushuru wa Samaki,
vi. Ushuru wa madini ya ujenzi,
vii. Ada ya kuendesha shughuli za utamaduni, burudani na michezo,
viii. Ada ya matangazo ya biashara,
ix. Ada ya upimaji wa ardhi na vibali vya ujenzi.
x. Ada na Ushuru wa minada.
xi. Ushuru wa kusafirisha mifugo.
xii. Ushuru wa masoko.
xiii. Ushuru wa Mazao ya misitu.
xiv. Ada na Ushuru kwa huduma nyingine

(4) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutokana na chanzo husika.

(5) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

(3) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa Ada na ushuru.

Uteuzi wa Wakala

6. (1) Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

(2) Wakala aliyeteuliwa chini ya sheria ndogo hizi atakuwa na wajibu wa;

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kusaini Mkataba.

(d) Kusanyo la mwezi mmoja lililowekwa dhamana na wakala litarejeshwa mwisho wa mwaka wa fedha unahusika na Mkataba.

(e) Kuilipa Halmashauri kiwango cha uwakala kilichokubaliwa katika mkataba siku tano (5) kabla ya tarehe ya kuanza uwakala Kwa kila mwezi;

(f) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

SEHEMU YA III
MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu

7. Itakuwa ni kosa kwa:-

(1) Kwa Wakala;

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;
(b) Atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;
(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi Hamsini elfu (50,000/=) au Kifungo cha miezi kumi na miwili jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Kwa yeyote;

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;
(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;
(c) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;
(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;
(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; Na
(f) Atamzuia Afisa Muidhiwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi Miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

8. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi Laki moja (100,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Jedwali la Nane la Sheria Ndogo hizi.

YAMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (1)

JEDWALI LA KWANZA

I. ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

Na.	*Huduma*	*Kiwango kwa siku*
1.	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe	Tshs 100,000/=
2.	Kukodi nyumba za Halmashauri	Kwa mujibu wa Mkataba
3.	Kukodi viti	Tshs 200/=
4.	Meza	Tshs 500/=
5.	Kukodi vibanda eneo la Soko la kojifa	Kwa mujibu wa Mkataba
6.	Kukodi vibanda eneo la Stendi la Benaco	Kwa mujibu wa Mkataba
7.	Lori	Tshs 350/= kwa kilometa
8.	Trekta	Tshs 60,000/= kwa saa

II. USHURU WA GARI LA KUNYONYA MAJI MACHAFU

Na.	*Huduma*	*Kiwango kwa tripu*
1.	Maeneo ya Mjini ndani ya Wilaya	Tshs 30,000/=
2.	Nje ya Mjini ndani ya Wilaya	Tshs 50,000/=
3.	Kukodi gari nje ya Wilaya	Tshs 400,000/=

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

III.ADA YA VIBANDA VYA BIASHARA

(a)Soko Kuu (Ngara Mjini)

Na.		*Kiwango kwa mwezi*
1.	Vibanda vya maduka soko la Ngara Mjini	Tshs 5,000/=
2.	Vibanda kituo cha Mabasi Ngara Mjini	Tshs 5,000/=
3.	Kituo cha mabasi Rulenga	Tshs 5,000/=
4.	Soko la Rulenga	Tshs 5,000/=
5.	Soko la Murusagamba	Tshs 5,000/=
6.	Eneo la Benaco center	Tshs 5,000/=
7.	Soko la Kabanga	Tshs 5,000/=
8.	Eneo la Rusumo Mpakani	Tshs 5,000/=

(b)Meza sokoni(meza sokoni)

Na.		*Kiwango*
1.	Meza za ndani	Tshs 200/=kwa siku
2.	Meza za samaki	Tshs 300/= kwa siku
3.	Meza za Samaki	Tshs 5,000/= kwa mwezi
4.	Wauza kuku	Tshs 5,000/= kwa mwezi
5.	Vibanda vingine vya biashara	Tshs 5,000/= kwa mwezi
6.	Bucha	Tshs 20,000/= kwa mwezi

IV.ADA YA UPIMAJI WA ARDHI

A.	***Ada ya Kibali ya Upimaji***	***Kwa kila kibali***
	1. K iwanja kidogo	280,000/=
	2. Kiwanja cha kati	360,000/=
	3. Kiwanja kikubwa	380,000/=
B.	***Gharama za kuandaa michoro ya mipango miji***	***Kwa kila mchoro***
	1. Ardhi inayomilikiwa chini ya watu 20	Tshs 1,500,000
	2. Ardhi inayomilikiwa na watu 20-50	Tshs 2,500,000
	3. Ardhi inayomilikiwa za zaidi ya watu 50	Kila atakayeongeza atalipa Tshs 50,000/=
C.	***Ada ya kuhakiki mipaka ya kiwanja***	
	1. Kiwanja kidogo(High Density)	Tshs 20,000/=
	2. Kiwanja cha kati(Medium Density)	Tshs 20,000/=
	3. Kiwanja kikubwa(Low Density)	Tshs 30,000/=
	4. Kiwanja kikubwa zaidi	Tshs 50,000/=

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

V.ADA YA USHURU WA MINADA

Na.	*Aina ya mnyama*	*Kiwango*
1.	N,gombe aliyeuzwa na muuzaji	Tshs 500/=kwa mmoja
2.	Ng,ombe aliyenunuliwa na muuzaji	Tshs 3,000/=kwa mmoja
3.	Mbuzi kwa aliyeuzwa na muuzaji	Tshs 3,00/=kwa mmoja
4.	Mbuzi aliyenunuliwa na mnunuzi	Tshs 1,000/=kwa mmoja
5.	Kondoo kwa aliyeuzwa na muuzaji	Tshs 3,00/=kwa mmoja
6.	Kondoo kwa aliyenunuliwa na mnunuzi	Tshs 1,000/=kwa mmoja

VI.ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA

Na.	*Ada/Ushuru*	*Kiwango*
1.	Ng'ombe atakayechinjwa	3,000/= kila mmoja
2.	Kondoo	1,000/= kila mmoja
3.	Mbuzi	1,000/= kila mmoja
4.	Nguruwe	1,000/= kila mmoja

VII.FAINI YA UINGIZAJI WA MIFUGO NDANI YA WILAYA

Na.	*Ada/Ushuru*	*Kiwango*
1.	Ng,ombe kutoka Wilaya jirani	Tshs 10,000 kwa Ng,ombe
2.	Ng,ombe kutoka nchi jirani	Tshs 50,000 kwa Ng,ombe

VIII.USHURU WA MAZAO YA SAMAKI

Na.		*Kiasi cha Ushuru*
1.	Gunia la dagaa	Tshs 1,000/=
1.	Samaki tenga moja	Tshs 3,000/=

IX.ADA NA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO KWA MAENEO YALIYOTENGWA

Na.	*Chombo cha usafiri*	*Ushuru wa maegesho*
1.	Gari dogo	500/= kwa siku
2.	Gari kubwa	2,500/= kwa siku
3.	Gari lenye uwezo wa kubeba watu2 hadi 10	200/= kwa saa 1
4.	Gari lenye uwezo wa kubeba watu 11 hadi 18	300/= kwa saa 1
5.	Magari ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 1hadi 4	300/= kwa saa 1

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

6.	Gari ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 5 hadi 7	500/= kwa saa 1
7.	Gari la mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 8 na kuendelee	1,000/= kwa saa 1
8.	Basi kubwa	2,000/= kwa siku
9.	Basi dogo	1,000/= kwa siku
10.	Taxii	500/= kwa siku`

X.USHURU WA MADINI YA UJENZI

Na.	*Aina ya madini ya Ujenzi*	*Kiasi cha Ushuru*
1.	Kokoto	
	(a)Lori dogo	Tshs 2,500/= kwa tipu
	(b)Lori kubwa	Tshs 5,000/= kwa tripu
2.	Mawe	
	(a)Lori dogo	Tshs 2,500/= kwa tripu
	(b)Lori kubwa	Tshs 5,000/= kwa tripu
3.	Mchanga	
	(a)Lori dogo	Tshs 2,500 kwa tripu
	(b)Lori kubwa	Tshs 5,000 kwa tripu
4.	Kifusi	
	(a)Lori dogo	Tshs 2,500 kwa tripu
	(b)Lori kubwa	Tshs 5,000 kwa tripu
5.	Tofari	Tshs 2 kwa tofali

XI.USHURU WA USAFIRISHAJI WA MAGARI KWA AJILI YA BIASHARA

Ndizi	Tshs 300/= kwa mkungu wa ndizi
Parachichi	Tshs 500/= kwa gunia
Bidhaa	Tshs 300/= kwa gunia

XII.ADA NA USHURU KWA AJILI YA SHUGHULI ZA UFUNDI

Fundi seremala	Tshs 5,000/= kwa mwezi
Fundi kuchomelea vyuma	Tshs 5,000/= kwa mwezi
Garage ya kukagua magari	Tshs 5,000/= kwa mwezi

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

Garage ya pikipiki	Tshs 2,000/= kwa mwezi

XIII.ADA YA MATANGAZO YA BIASHARA

	Aina ya tangazo	***Kiwango cha ushuru***
1.	Matangazo ambayo yataandikwa kwenye vibao na kuwekwa barabarani katika eneo la mji	
	(a)ambayo siyo yenye kutoa mwanga	Tshs 15,000/= kwa mwaka
	(b)yenye kutoa mwanga	Tshs 20,000/= kwa mwaka
2.	Matangazo ambayo yataandikwa kwenye vibao na kuwekwa nje ya eneo la mji.	
	(a)ambayo hayatoi mwanga	Tshs 10,000/= kwa mwaka
	(b)yenye kutoa mwanga	Tshs 15,000 /= kwa mwaka

XIV.USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

	Aina ya mazao	***Kiwango cha ushuru***
1.	Mkaa(gunia)	1,000/= kwa gunia
2.	Mbao(bila kujali unene)	200/= kwa gunia
3.	Nguzo(biola kujali unene)	300/= kwa nguzo
4.	Asali(debe)	1,000/= kwa debe
5.	Nta(kwa kilo)	200/=
6.	Fito moja	100/=
7.	Kuni(mita ya ujazo)	1,000/=
8.	Biashara kutokana na zao la ukindu au katani(mkeka mmoja)	200/=
9.	Matunda ya miti(mibuyu,ukwaju,na pasheni)debe moja	200/=
10.	Mipini,upinde kila mmoja	100/=
11.	Vinu na mitwangio kila moja	100/=

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

XV.ADA YA MAOMBI YA VIBALI VYA MABADILIKO YA ARDHI

Na.		*Kiwango kwa kibali*
1.	Kutoka kundi lolote kwenda taasisi	Tshs 50,000/=
2.	Kutoka kundi lolote kwenda biashara	Tshs 50,000/=
3.	Kutoka kundi lolote kwenda wiwanda au kituo cha mafuta	Tshs 70,000/=
4.	Kutoa kundi lolote kwenda garage	Tshs 70,000/=
5.	Maombi ya kugawa viwanja	Tshs 100,000/=
6.	Kondoo kwa aliyenunuliwa na mnunuzi	Tshs 1,000/=kwa mmoja

XVI.ADA YA UKAGUZI WA RAMANI

Na.	*Aina ya Ukaguzi*	*Kiwango*
1.	Jengo la biashara	Tshs 25,000/=
2.	Jengo la biashara na makazi	Tshs 25,000/=
3 .	Jengo la Makazi	Tshs 15,000/=

MASOKO YA HALMASHAURI NA MAHALI YALIPO

S/NA	JINA LA SOKO	MAHALI LILIPO
1.	Ngara Mjini	Mamlaka ya Mji mdogo wa Ngara
2.	Mayenzi	Kijiji cha Mayenzi
3.	Nyakiziba	Kijiji cha Nyakiziba
4.	Rwabilulu	Kijiji cha Rusumo
5.	Kasulo	Kijiji cha Kasulo
6.	Kabalenzi	Kijiji cha Kabalenzi
7.	Kanazi	Kijiji cha Kanazi
8.	Kabanga	Kijiji cha Kabanga

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

9.	Djululigwa	Kijiji cha Djululigwa
10.	Muhweza	Kijiji cha Muhweza
11.	Mugoma	Kijiji cha mugoma
12.	Mumwendo	Kijiji cha Kumwendo
13.	Rulenge	Kijiji cha Rulenge
14.	Mbuba	Kijiji cha Mbuba
15.	Kanyinya	Kijiji cha Kanyinya
16.	Keza	Kijiji cha Keza
17.	Bukiriro	Kijiji cha Bukiriro
18.	Bugarama	Kijiji cha Bugarama
19.	Mukalinzi	Kijiji cha Mukalinzi
20.	Murusagamba	Kijiji cha Murusagamba
21.	Ntanga	Kijiji cha Ntanga
22.	Ntobeye	Kijiji cha Ntobeye
23.	Lukole	Kijiji cha Kasulo
24.	Nyarulama	Kijiji cha Nyarulama
25.	Nyakisasa	Kijiji cha Nyaulama
26.	Ruyigi	Kijiji cha Nyakisasa
27.	Nyamahwa	Kijiji cha Bukiriro
28.	Kashinga	Kijiji cha Nyamahwa

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

29.	Murunyinya	Kijiji cha Nyakiziba
30.	Mikole	Kijiji cha Nyamahwa

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 8)

Mimi …… nakiri mbele ya …….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Ngara, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Ngara (Ada na Ushuru) za Mwaka 2014.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……. .ya Mwezi……..…… Mwaka …….

Jina……..…… *Saini*…….

Mbele ya :

Jina: ……

Cheo: …….…….

Saini: …….……..

Tangazo la serikali na. 435 (linaendelea)

Sheria Ndogo hizi zimetungwa kwa Azimio la Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 5 mwezi Mei 2013 na Mhuri wa Halmashauri umebandikwa mbele ya:-

JOHN M. SHIM'IMANA
Mwenyekiti Halmashauri Wilaya ya Ngara

CORNEL E. NGUDU-NGI
Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Ngara

NAKUBALI

Dodoma
27 Juni, 2014

MIZENGO P. PINDA (MB),
Waziri Mkuu